



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## UTAFITI WA MWAKA WA UZALISHAJI VIWANDANI 2015 na 2016

### MUHTASARI WA MATOKEO



Oktoba 2018

# **YALIYOMO**

<b>Orodha ya Majedwali .....</b>	<b>iii</b>
<b>Orodha ya Michoro.....</b>	<b>iv</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>1.0 Utangulizi.....</b>	<b>1</b>
<b>Sura ya pili.....</b>	<b>3</b>
<b>2.0 Aina ya Viwanda .....</b>	<b>3</b>
2.1 Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda.....	3
2.2 Idadi ya Viwanda kwa Shughuli za Uzalishaji Viwandani.....	4
2.3 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa.....	5
2.4 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi.....	6
2.5 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Aina ya Umiliki.....	7
2.6 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana naMsingi wa Umiliki Kisheria .....	8
2.7 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Asilia/Utaifa wa Wamiliki .....	8
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>9</b>
<b>3.0 Idadi ya Wafanyakazi Viwandani .....</b>	<b>9</b>
3.1 Idadiya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda .....	9
3.2 Idadi ya Wafanyakazi Kijinsia Katika Sekta Ndogo za Viwanda.....	10
3.3 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Shughuli za Viwanda .....	10
3.4 Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani .....	12
3.5 Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi .....	14
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>15</b>
<b>4.0 Malipo kwa Wafanyakazi.....</b>	<b>15</b>
4.1 Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda .....	15



**SURA YA TANO .....**.....**17**

**5.0      Ongezeko la Thamani .....**.....**17**

5.1	Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo za Viwanda .....	17
5.2	Ongezeko la Thamani Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kwa Shughuli za Viwanda .....	18
5.3	Ongezeko la Thamani katika Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi. ....	20
5.4	Ongezeko la Thamani katika Sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa.....	21



## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1:	Idadi ya Viwanda Katika Shughuli za Uzalishaji Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016 .....	5
Jedwali Na. 2:	Idadi ya Viwanda katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	6
Jedwali Na. 3:	Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Aina ya Umiliki, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	7
Jedwali Na. 4:	Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Asilia/Utaifa wa Wamiliki, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	8
Jedwali Na. 5:	Idadiya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	9
Jedwali Na. 6:	Idadi ya Wafanyakazi Kijinsi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	10
Jedwali Na. 7:	Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Shughuli za Viwanda.....	12
Jedwali Na. 8:	Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa viwandani Ki-Mkoa, ASIP 2015 na 2016.....	13
Jedwali Na. 9:	Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016 .....	14
Jedwali Na. 10:	Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	15
Jedwali Na. 11:	Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2015 .....	19
Jedwali Na. 12:	Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2016 .....	20
Jedwali Na. 13:	Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani (MVA) Ki-Mkoa, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.....	22



## **Orodha ya Michoro**

Mchoro Na. 1:	Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda , Tanzania Bara .....	3
Mchoro Na. 2:	Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016 .....	7
Mchoro Na. 3:	Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016. ....	17
Mchoro Na. 4:	Mgawanyo wa Ongezeko la Thamani Katika Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara. ....	21



# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekekezaji (MITI) ilifanya Utafiti wa mwaka wa Uzalishaji Viwandani kwa miaka rejea ya 2015 na 2016.

Utaditi huu umefanyika kwa msaada wa kiufundi uliotolewa na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) na fedha zilitolewa na Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo kuititia fungu linalotolewa kwa ajili ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania (Tanzania Statistical Master Plan - TSMP).

Lengo kuu la Utafiti wa mwaka wa Uzalishaji Viwandani lilikuwa ni kutoa taarifa sahihi zinazohusu sekta ya viwanda na ambazo zitatumika katika kutathmini mchango wa sekta ya viwanda kwa uchumi wa Nchi. Aidha, sensa ilikuwa na lengo la kutoa taarifa za msingi ambazo zitatumika kufanikisha tafiti nyingine na kuwezesha uchambuzi wa mipango mbalimbali, utungaji wa sera na kusaidia katika kufanya maamuzi sahihi.

Utafiti wa mwaka wa Uzalishaji Viwandani kwa mika rejea 2015 na 2016 umehusisha viwanda vyote vyenye maeneo ya kudumu Tanzania Bara kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Mgawanyo wa Shughuli za Uzalishaji na Utoaji Huduma (ISIC) toleo Namba 4 ili kuhakikisha ulinganishi kimataifa. Utafiti imejumuisha viwanda vyote vilivyojishughulisha na Uchimbaji madini na mawe; Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani; Uzalishaji na usambazaji wa Umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi); na Kukusanya, kutibu na kusambaza maji.

Utengenezaji wa bidhaa viwandani unahusu ubadilishaji wa malighafi kuwa bidhaa mpya kwa kubadilisha muundo na maumbo. Bidhaa zinazobadilishwa ni malighafi ambazo zinatokana na kilimo, misitu, uvuvi, uchimbaji madini na mawe pamoja na bidhaa za shughuli nyingine za utengenezaji wa bidhaa viwandani ambazo ni malighafi kwa sekta hii. Shughuli za ubadilishaji, urekebishaji wa bidhaa pia hutambulika kama utengenezaji wa bidhaa viwandani.

Madhumuni ya ripoti hii ni kuwasilisha kwa muhtasari, matokeo muhimu yanayohusu Utafiti wa mwaka wa Uzalishaji Viwandani kwa miaka rejea 2015 na 2016 ili kutoa rejea muhimu juu ya nini kinapatikana kwenye ripoti kuu. Ripoti imetoea kwa ufupi, matokeo

muhimu yanayohusu aina na mifumo mbalimbali ya viwanda husika, ajira na malipo yake, pato ghafi, gharama za uzalishaji na ongezeko la thamani. Matokeo haya yamegawanyika kulingana na aina ya uzalishaji, ukubwa wa kiwanda kulingana na idadi ya wafanyakazi, eneo la kijiografia mahali kiwanda kilipo na hali ya umiliki.

# SURA YA PILI


## 2.0 Aina ya Viwanda

### 2.1 Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Mwaka 2015 jumla ya viwanda vilivyofanya uzalishaji vilikuwa 2,389. Kati ya viwanda 2,389 , sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani ilikuwa na viwanda vingi (1,864, asilimia 78.0) kuliko sekta ndogo yoyote, ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe viwanda (384, asilimia 16.1), kukusanya, kutibu na kusambaza maji viwanda (110, asilimia 4.6) na ya mwisho ilikuwa uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) ambayo ilikuwa na viwanda(31, asilimia 1.3).

Kwa mwaka 2016 jumla ya viwanda vilivyofanya uzalishaji vilikuwa 2,462. Kati ya viwanda 2,462 , sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani ilikuwa na viwanda vingi (1,931, asilimia 78.4) kuliko sekta ndogo yoyote, ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe viwanda (385, asilimia 15.6), kukusanya, kutibu na kusambaza maji viwanda (110, asilimia 4.5) na ya mwisho ilikuwa uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) ambayo ilikuwa na viwanda(36, asilimia 1.5).

Mchoro Na. 1: Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda , Tanzania Bara



*Kutokana na Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya mwaka rejea 2013 jumla ya viwanda vilivyokuwa na wafanyakazi kumi au zaidi vilikuwa 1,322, kati ya hivyo sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa na viwanda 998 ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe viwanda 210. Kutoka mwaka 2013 hadi 2016 kulikuwa na ongezeko la viwanda 933 katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani vyenye wafanyakazi kumi au zaidi.*

## **2.2 Idadi ya Viwanda kwa Shughuli za Uzalishaji Viwandani**

Idadi ya viwanda kwa kila shughuli ya uzalishaji hutofautiana kutoka shughuli moja hadi nyingine. Katika mwaka 2015 shughuli nne za uzalishaji zilizoongoza zimechangia asilimia 69.4 ya jumla ya idadi ya viwanda, nazo ni: utengenezaji wa bidhaa za chakula viwanda (751, asilimia 40.3); utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali (216, asilimia 11.6); utengenezaji wa samani (198, asilimia 10.6); na utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia (128, asilimia 6.9).

Kwa mwaka 2016 shughuli nne za uzalishaji zilizoongoza zimechangia asilimia 69.2 ya jumla ya idadi ya viwanda, nazo ni: utengenezaji wa bidhaa za chakula viwanda (803, asilimia 41.6); utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali (222, asilimia 11.5); utengenezaji wa samani (195, asilimia 10.1); na utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia (116, asilimia 6.0).

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Viwanda Katika Shughuli za Uzalishaji Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**

Shughuli ya Kiwanda	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Utengenezaji wa bidhaa za chakula	751	40.3	803	41.6
Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali	216	11.6	222	11.5
Utengenezaji wa samani	198	10.6	195	10.1
Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia	128	6.9	116	6.0
Utengenezaji wa vinywaji	71	3.8	67	3.5
Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa	69	3.7	78	4.0
Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa	58	3.1	60	3.1
Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali	55	3.0	55	2.8
Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki	55	3.0	58	3.0
Utengenezaji wa nguo	50	2.7	42	2.2
Utengenezaji wa metali za msingi	47	2.5	48	2.5
Utengenezaji mwingine wa bidhaa vya viwandani	43	2.3	45	2.3
Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana	27	1.4	28	1.5
Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa	15	0.8	14	0.7
Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi	14	0.8	16	0.8
Utengenezaji wa mavazi	13	0.7	18	0.9
Utengenezaji wa vifaa vya umeme	13	0.7	23	1.2
Utengenezaji wa magari na matela ya malori	12	0.6	14	0.7
Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa	11	0.6	8	0.4
Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea	5	0.3	6	0.3
Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku	4	0.2	4	0.2
Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa	4	0.2	4	0.2
Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri	3	0.2	3	0.2
Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni	2	0.1	4	0.2
	<b>1,864</b>	<b>100.0</b>	<b>1,931</b>	<b>100.0</b>

### 2.3 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa

Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwani vilivyozalisha katika mwaka 2015 ikiwa na viwanda 527 (asilimia 28.3%) , ukifutiwa na mikoa ya Morogoro 232 (asilimia 12.4); Arusha 140 (asilimia 7.5) na Kilimanjaro viwanda 98 (asilimia 5.3). Hata hivyo, Mkoa wa Geita ulikuwa na idadi ndogo ya viwanda 8 (asilimia 0.4).

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Viwanda katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**

Mkoa	Jumla		Sekta Ndogo ya Utengenezaji Wa Bidhaa Viwandani		Sekta Ndogo Zinginez	
	2015	2016	2015	2016	2015	2016
Dodoma	50	57	43	50	7	7
Arusha	144	143	140	139	4	4
Kilimanjaro	115	99	98	83	17	16
Tanga	58	62	47	51	11	11
Morogoro	239	245	232	238	7	7
Pwani	64	80	57	68	7	12
Dar es Salaam	535	542	527	530	8	12
Lindi	20	25	13	17	7	8
Mtwara	26	28	19	21	7	7
Ruvuma	28	32	19	24	9	8
Iringa	34	35	30	31	4	4
Mbeya	89	88	64	61	25	27
Singida	91	93	63	66	28	27
Tabora	13	11	11	9	2	2
Rukwa	41	41	34	35	7	6
Kigoma	75	76	67	67	8	9
Shinyanga	65	67	51	54	14	13
Kagera	49	54	44	49	5	5
Mwanza	84	88	79	84	5	4
Mara	91	95	54	59	37	36
Manyara	352	352	70	73	282	279
Njombe	12	16	11	14	1	2
Katavi	23	35	21	33	2	2
Simiyu	54	56	45	46	9	10
Geita	16	20	8	12	8	8
Songwe	21	22	17	17	4	5
<b>Jumla</b>	<b>2,389</b>	<b>2,462</b>	<b>1,864</b>	<b>1,931</b>	<b>525</b>	<b>531</b>

Pia mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwani vilivyozalisha katika mwaka 2016 ikiwa na viwanda 530 (asilimia 27.4%) , ukifuatiwa na mikoa ya Morogoro 238 (asilimia 12.3); Arusha 139 (asilimia 7.2) na Kilimanjaro viwanda 83 (asilimia 4.3). Hata hivyo, Mkoa wa Geita ulikuwa na idadi ndogo ya viwanda 12 (asilimia 0.6).


#### **2.4 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi**

Mwaka 2015 kundi lenye wafanyakazi kuanzia kumi hadi kumi na tisa (10 – 19) lilikuwa na idadi kubwa zaidi ya viwanda vya utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ambavyo ni 1,085 sawa na asilimia 58.2, likifuatiwa na kundi lenye wafanyakazi kuanzia ishirini hadi arobaini na tisa (20 – 49) lenye viwanda 405 sawa na asilimia 21.7.



Pia katika mwaka 2016 kundi lenye wafanyakazi kuanzia kumi hadi kumi na tisa (10 – 19) lilikuwa na idadi kubwa zaidi ya viwanda vya utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ambavyo ni 1,131 sawa na asilimia 58.6, likifuatiwa na kundi lenye wafanyakazi kuanzia ishirini hadi arobaini na tisa (20 – 49) lenye viwanda 418 sawa na asilimia 21.6.

**Mchoro Na. 2: Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**



## 2.5 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Aina ya Umiliki

Kwa mwaka 2015 kutoka jumla ya viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani 1,864, viwanda 1,769 sawa na asilimia 94.9 vilimilikiwa na mashirika binafsi, viwanda 72 sawa na asilimia 3.9 vilimilikiwa na Serikali, wakati viwanda 23 sawa na asilimia 1.2 vilimilikiwa kwa ubia kati ya Serikali na Mashirika Binafsi.

Wakati kwa mwaka 2016 kutoka jumla ya viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani 1,931, viwanda 1,825 sawa na asilimia 94.5 vilimilikiwa na mashirika binafsi, viwanda 81 sawa na asilimia 4.2 vilimilikiwa na Serikali, wakati viwanda 25 sawa na asilimia 1.3 vilimilikiwa kwa ubia kati ya Serikali na Mashirika Binafsi.

**Jedwali Na. 3: Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Aina ya Umiliki, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.**

Aina ya Umiliki	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Serikali	72	3.9	81	4.2
Mashirika Binafsi	1,769	94.9	1,825	94.5
Ubia Serikali na Mashirika Binafsi	23	1.2	25	1.3
<b>Jumla</b>	<b>1,864</b>	<b>100</b>	<b>1,931</b>	<b>100</b>

## **2.6 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana naMsingi wa Umiliki Kisheria**

Kuendana na msingi wa umiliki wa kisheria, matokeo yanaonesha kuwa, kwa mwaka 2015 katika jumla ya viwanda 1,864 vya Utengenezaji wa Bidhaa viwandani , umiliki wa mtu mmoja ulikuwa na viwanda 795 sawa na asilimia 42.7, ikifuatiwa na mashirika binafsi yenyе hisa za dhima isiyo na ukomo, viwanda 543 (asilimia 29.1) na Ubia viwanda 238 (asilimia 12.8).

Wakati kwa mwaka 2016 kuendana na msingi wa umiliki wa kisheria, matokeo yanaonesha kuwa, katika jumla ya viwanda 1,931 vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, umiliki wa mtu mmoja ulikuwa na viwanda 805 sawa na asilimia 41.7, ikifuatiwa na mashirika binafsi yenyе hisa za dhima isiyo na ukomo, viwanda 557 (asilimia 28.8) na mashirika binafsi yenyе hisa za dhima isiyo na ukomo, na Ubia viwanda 238 (asilimia 13.8).

## **2.7 Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Asilia/Utaifa wa Wamiliki**

Katika asilia/utaifa wa wamiliki, matokeo yanaonyesha kuwa, katika mwaka 2015 kutoka jumla ya viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani 1,864, viwanda 1,594 sawa na asilimia 85.5 vilimikiwa na Wazawa/Watanzania, viwanda vilivyomilikiwa na wageni kutoka mataifa ya nje vilikuwa 186 sawa na asilimia 10.0 na vilivyomilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wa Nje vilikuwa 84 sawa na asilimia 4.5

Wakati kwa mwaka 2016 katika asilia/utaifa wa wamiliki, matokeo yanaonyesha kuwa, kutoka jumla ya viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani 1,931, viwanda 1,654 sawa na asilimia 85.7 vilimikiwa na Wazawa/Watanzania, viwanda vilivyomilikiwa na wageni kutoka mataifa ya nje vilikuwa 198 sawa na asilimia 10.3 na vilivyomilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wa Nje vilikuwa 79 sawa na asilimia 4.1

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kulingana na Asilia/Utaifa wa Wamiliki, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.**

Asilimia/Utaifa wa Mmiliki	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Mzawa/Mtanzania	1,594	85.5	1,654	85.7
Kutoka Nje ya Tanzania	186	10	198	10.3
Ubia Mzawa na wa Nje	84	4.5	79	4.1
<b>Jumla</b>	<b>1,864</b>	<b>100</b>	<b>1,931</b>	<b>100</b>

# SURA YA TATU

## 3.0 Idadi ya Wafanyakazi Viwandani

### 3.1 Idadiya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Mwaka 2015 matokeo yanaonesha kuwa, idadi ya wafanyakazi katika sekta ndogo nne ilikuwa 201,343; kati ya hao, wafanyakazi wa viwanda vilivyojihusisha na utengenezaji wa bidhaa viwandani walikuwa 156,579 (asilimia 77.8), ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe yenye wafanyakazi 31,734 (asilimia 15.8).

Katika mwaka 2016 matokeo yanaonesha kuwa, idadi ya wafanyakazi katika sekta ndogo nne ilikuwa 221,688; kati ya hao, wafanyakazi wa viwanda vilivyojihusisha na utengenezaji wa bidhaa viwandani walikuwa 177,173 (asilimia 79.9), ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe yenye wafanyakazi 30,472 (asilimia 13.7).

**Jedwali Na. 5: Idadiya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**

Sekta Ndogo	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Uchimbaji Madini na Mawe	31,734	15.8	30,472	13.7
Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani	156,579	77.8	177,173	79.9
Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme, Gesi				
Mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi)	3,985	2.0	4,532	2.0
Kukusanya, kutibu na kusambaza maji	9,045	4.5	9,511	4.3
<b>Jumla</b>	<b>201,343</b>	<b>100</b>	<b>221,688</b>	<b>100</b>

*Matokeo ya Sensa ya Viwanda kwa mwaka rejea 2013, idadi ya wafanyakazi katika Sekta Ndogo nne kwa viwanda vilivyojiri wafanyakazi kumi au zaidi 910+) ilikuwa 138,887, kati ya hao Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa na wafanyakazi 107,732 (asilimia 78.6) ikifuatiwa na sekta ndogo ya Uchimaji Madini na Mawe ambayo ilikuwa na wafanyakazi 18,917 (asilimia 14.6).*

*Kutoka mwaka 2013 hadi 2016 kulikuwa na ongezeko la wafanyakazi 69,441 katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa viwanda vilivyokuwa na wafanyakazi kumi au zaidi.*

### **3.2 Idadi ya Wafanyakazi Kijinsia Katika Sekta Ndogo za Viwanda**

Matokeo yanaonesha kuwa, katika mwaka 2015 viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi; sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 93.8 na wanawake asilimia 6.2; sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 69.9 na wanawake asilimia 30.1; sekta ndogo ya umeme, gesi, mvuke na hali ya hewa ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 83.6 na wanawake asilimia 16.4; na sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji, ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 80.3 na wanawake asilimia 19.7.

Katika mwaka 2016, sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 93.1 na wanawake asilimia 6.9; sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 67.0 na wanawake asilimia 33.0; sekta ndogo ya umeme, gesi, mvuke na hali ya hewa ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 86.7 na wanawake asilimia 13.3; na sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji, ilikuwa na wafanyakazi wanaume asilimia 79.9 na wanawake asilimia 20.1.

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Wafanyakazi Kijinsi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.**

Sekta Ndogo	2015			2016		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Uchimbaji Madini na Mawe	29,781	1,962	31,743	28,380	2,092	30,472
Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani	109,440	47,139	156,579	118,710	58,463	177,173
Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme, Gesi						
Mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi)	3,331	654	3,985	3,929	603	4,532
Kukusanya, kutibu na kusambaza maji	7,262	1,783	9,045	7,599	1,912	9,511
<b>Jumla</b>	<b>149,814</b>	<b>51,538</b>	<b>201,352</b>	<b>158,618</b>	<b>63,070</b>	<b>221,688</b>

### **3.3 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Shughuli za Viwanda**

Idadi ya wafanyakazi katika shughuli za viwanda hutofautiana kutoka shughuli moja hadi nyingine. Katika mwaka 2015 ambapo idadi ya wafanyakazi katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa 156,579, shughuli kuu tatu za viwanda zilizoongoza kwa idadi kubwa ya wafanyakazi ziliikuwa kama ifuatavyo: utengenezaji wa

bidhaa za chakula, wafanyakazi 63,579 sawa na asilimia 40.6, utengenezaji wa vinywaji, wafanyakazi 13,354 sawa na asilimia 8.5, na utengenezaji wa mavazi 12,406 sawa na asilimia 7.9. Shughuli nyingine za viwanda zimechangia asilimia 43.0 ya wafanyakazi wote.

Mwaka 2016 idadi ya wafanyakazi katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa 177,173, shughuli kuu tatu za viwanda zilizoongoza kwa idadi kubwa ya wafanyakazi zilikuwa kama ifuatavyo: utengenezaji wa bidhaa za chakula, wafanyakazi 78,746 sawa na asilimia 44.4, utengenezaji wa vinywaji, wafanyakazi 17,835 sawa na asilimia 10.1, na utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali 11,897 sawa na asilimia 6.7. Shughuli nyingine za viwanda zimechangia asilimia 38.8 ya wafanyakazi wote.

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Shughuli za Viwanda**

Shughuli ya Kiwanda	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Utengenezaji wa bidhaa za chakula	63,579	40.6	78,746	44.4
Utengenezaji wa vinywaji	13,354	8.5	17,835	10.1
Utengenezaji wa nguo	12,406	7.9	9,068	5.1
Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali	10,152	6.5	11,897	6.7
Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali	7,584	4.8	7,719	4.4
Utengenezaji wa samani	7,079	4.5	6,705	3.8
Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku	5,863	3.7	4,372	2.5
Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia	5,379	3.4	4,522	2.6
Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki	5,241	3.3	5,032	2.8
Utengenezaji mwingine wa bidhaa vya viwandani	4,265	2.7	6,177	3.5
Utengenezaji wa metali za msingi	3,519	2.2	3,786	2.1
Utengenezaji wa mavazi	2,749	1.8	4,194	2.4
Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa	3,212	2.1	3,613	2
Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi	2,664	1.7	2,695	1.5
Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa	2,211	1.4	2,870	1.6
Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana	1,637	1.0	2,544	1.4
Utengenezaji wa vifaa vya umeme	1,444	0.9	1,379	0.8
Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea	987	0.6	1,206	0.7
Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri	958	0.6	461	0.3
Utengenezaji wa magari na matela ya malori	930	0.6	1,000	0.6
Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa	520	0.3	537	0.3
Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa	396	0.3	352	0.2
Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyo safishwa	293	0.2	259	0.1
Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni	157	0.1	204	0.1
<b>Jumla</b>	<b>156,579</b>	<b>100</b>	<b>177,173</b>	<b>100</b>

### 3.4 Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani

Kutokana na jumla ya wafanyakazi 156,579 katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa mwaka 2015, mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi kuliko mikoa mingine ambao ni wafanyakazi 51,493 (asilimia 32.9)



ikifuatiwa na Morogoro, 23,605 (asilimia 15.1). Mkoa wa Geita ulikuwa na idadi ndogo ya wafanyakazi kuliko mikoa mingine kwa kuwa na wafanyakazi ambao ni 326 (asilimia 0.2).

**Jedwali Na. 8: Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa viwandani Ki-Mkoa, ASIP 2015 na 2016**

Mkoa	2015		2016	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Dar es Salaam	51,493	32.9	57,167	32.3
Morogoro	23,605	15.1	26,710	15.1
Arusha	13,289	8.5	15,037	8.5
Kilimanjaro	9,979	6.4	11,291	6.4
Mwanza	7,959	5.1	9,370	5.3
Pwani	6,893	4.4	8,314	4.7
Tanga	6,421	4.1	8,523	4.8
Iringa	4,539	2.9	4,251	2.4
Mbeya	4,499	2.9	5,091	2.9
Manyara	3,720	2.4	4,367	2.5
Kagera	2,966	1.9	3,060	1.7
Mara	2,916	1.9	3,002	1.7
Shinyanga	2,245	1.4	2,349	1.3
Njombe	2,065	1.3	2,337	1.3
Mtewara	2,012	1.3	2,472	1.4
Dodoma	1,873	1.2	1,917	1.1
Singida	1,869	1.2	1,970	1.1
Kigoma	1,588	1	1,597	0.9
Ruvuma	1,344	0.9	1,595	0.9
Simiyu	1,316	0.8	1,489	0.8
Rukwa	1,289	0.8	1,312	0.7
Katavi	800	0.5	1,211	0.7
Songwe	663	0.4	750	0.4
Tabora	554	0.4	627	0.4
Lindi	356	0.2	853	0.5
Geita	326	0.2	511	0.3
<b>Jumla</b>	<b>156,579</b>	<b>100</b>	<b>177,173</b>	<b>100</b>

Katika mwaka 2016, Kutokana na jumla ya wafanyakazi 177,173 katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani , mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi kuliko mikoa mingine ambao ni wafanyakazi 57,167 (asilimia 32.3) ikifuatiwa na Morogoro, 26,710 (asilimia 15.1). Mkoa wa Geita ulikuwa na idadi ndogo ya wafanyakazi kuliko mikoa mingine kwa kuwa na wafanyakazi ambao ni 311 (asilimia 0.2).

### **3.5 Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi**

Mwaka 2015 viwanda vyenye wafanyakazi mia tano au zaidi 500+ vilikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi 52,782 (asilimia 33.7) vikifuatiwa na viwanda vyenye wafanyakazi mia moja hadi mia nne tisini na tisa (100 – 499) vilikuwa na wafanyakazi 50,194 (asilimia 32.1) na viwanda vyenye wafanyakazi kumi hadi kumi na tisa vilikuwa na jumla ya wafanyakazi 20,127 (asilimia 12.9).

Katika mwaka 2016, kutokana na jumla ya wafanyakazi katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, viwanda vyenye wafanyakazi mia tano au zaidi 500+ vilikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi 56,619 (asilimia 32.0) vikifuatiwa na viwanda vyenye wafanyakazi mia moja hadi mia nne tisini na tisa (100 – 499) vilikuwa na wafanyakazi 51,072 (asilimia 28.8) na viwanda vyenye wafanyakazi ishirini hadi kumi arobaini na tisa vilikuwa na jumla ya wafanyakazi 32,994 (asilimia 18.6).

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Wafanyakazi katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani katika Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**

Makundi ya Wafanyakazi	2015		2016	
	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>
<b>10 - 19</b>	20,127	12.9	20,255	11.4
<b>20 – 49</b>	16,454	10.5	32,994	18.6
<b>50 - 99</b>	17,022	10.9	16,233	9.2
<b>100 – 499</b>	50,194	32.1	51,072	28.8
<b>500+</b>	52,782	33.7	56,619	32.0
<b>Jumla</b>	<b>156,579</b>	<b>100</b>	<b>177,173</b>	<b>100</b>

# SURA YA NNE

## 4.0 Malipo kwa Wafanyakazi

### 4.1 Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Malipo kwa wafanyakazi yanahu su jumla ya malipo kwa wafanyakazi wote kwa fedha taslimu au fadhila, yanajumuisha mishahara, malipo ya muda wa ziada, gharama za usafiri, michango kwa mfanyakazi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo ya ziada kwa kuchangia uzalishaji katika kipindi husika.

Matokeo yameonesha kuwa, jumla ya malipo kwa wafanyakazi viwandani mwaka 2015 yalifiki Shilingi milioni 1,593,948. Malipo makubwa zaidi yalitolewa katika sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani yaliyogharimu Shilingi milioni 982,563; yakifuatiwa na sekta ndogo ya madini na uchimbaji mawe Shillingi millioni 448,770 na Sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji ilikuwa na malipo madogo kwa wafanyakazi yaligharimu Shilingi milioni 74,092.

Katika mwaka 2016, matokeo yameonesha kuwa, jumla ya malipo kwa wafanyakazi viwandani yalifiki Shilingi milioni 2,123,142. Malipo makubwa zaidi yalitolewa katika sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani yaliyogharimu Shilingi milioni 1,569,805; yakifuatiwa na sekta ndogo ya madini na uchimbaji mawe Shillingi millioni 368,274 na Sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji ilikuwa na malipo madogo kwa wafanyakazi yaligharimu Shilingi milioni 50,043.

**Jedwali Na. 10: Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.**

Sekta Ndogo	2015		2016	
	Kiasi (Mill. TZS)	Asilimia	Kiasi (Mill. TZS)	Asilimia
Uchimbaji Madini na Mawe	448,770	28.2	368,274	17.3
Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani	982,563	61.6	1,569,805	73.9
Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi)	88,523	5.6	135,020	6.4
Kukusanya, kutibu na kusambaza maji	74,092	4.6	50,043	2.4
<b>Jumla</b>	<b>1,593,948</b>	<b>100</b>	<b>2,123,142</b>	<b>100</b>





# SURA YA TANO

## 5.0 Ongezeko la Thamani


Ongezeko la Thamani ni mrejesho unaotokana na shughuli za uzalishaji mali, ambao ni tofauti kati ya Pato Ghafi (Gross Output) na Gharama za Uzalishaji (Intermediate Consumption). Ni kipimo cha mchango wa kiwanda husika katika Pato la Taifa (Gross Domestic Product - GDP).

### 5.1 Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo za Viwanda

Mwaka 2015 matokeo yanaonesha kuwa, jumla ya ongezeko la thamani kwa sekta yote ya viwanda ni Shilingi milioni 9,667,575. Viwanda Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa kiasi kikubwa cha ongezeko la thamani cha shilingi milioni 5,575,510 sawa na asilimia 57.7 ikifuatiwa na sekta ndogo ya Uchimbaji wa Madini na Mawe shilingi milioni 2,787,932 sawa na asilimia 28.8.

Wakati katika mwaka 2016, matokeo yanaonesha kuwa, jumla ya ongezeko la thamani kwa sekta yote ya viwanda ni Shilingi milioni 11,143,918. Viwanda Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani ilikuwa kiasi kikubwa cha ongezeko la thamani cha shilingi milioni 7,576,681 sawa na asilimia 68.0 ikifuatiwa na sekta ndogo ya Uchimbaji wa Madini na Mawe shilingi milioni 2,592,680 sawa na asilimia 23.3.

**Mchoro Na. 3: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016.**



*Matokeo ya Sensa ya Viwanda kwa mwaka rejea 2013 kwa viwanda viliwyokuwa na wafanyakazi kumi au zaidi (10+) yalionyesha kuwa, Ongezeko la Thamani lilikuwa shilingi milioni 7,857,680 kati ya kiasi hicho Ongezeko la Thamani katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani lilikuwa shilingi milioni 4,552,716 ikifuatiwa sekta ndogo ya Uchimbaji wa Madini na Mawe shilingi milioni 2,915,516.*

*Kutoka mwaka 2013 hadi 2016 kulikuwa na Ongezeko la Thamani la shilingi milioni 3,023,965 katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa viwanda viliwyokuwa na wafanyakazi kumi au zaidi (10+).*

## **5.2 Ongezeko la Thamani Katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Kwa Shughuli za Viwanda**

Ongezeko la thamani lilitofautiana kati ya shughuli moja hadi nyingine. Kutokana na jumla ya Ongezeko la Thamani katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa bidhaa viwandani ya shilingi milioni 5,575,510 ya mwaka 2015, shughuli zinazoongoza zenye Ongezeko la Thamani kubwa ni Utengenezaji wa bidhaa za chakula yenye shilingi milioni 1,235,537 ikifuatiwa na Utengenezaji wa vinywaji shilingi milioni 1,089,337, Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali shilingi milioni 522,382, Utengenezaji wa Bidhaa za Tumbaku shilingi milioni 454,690.

Katika mwaka 2016, kutokana na jumla ya Ongezeko la Thamani katika sekta ndogo ya Utengenezaji wa bidhaa viwandani ya shilingi milioni 7,576,681, shughuli zinazoongoza zenye Ongezeko la Thamani kubwa ni Utengenezaji wa Bidhaa za Chakula yenye shilingi milioni 2,596,278 ikifuatiwa na Utengenezaji wa vinywaji shilingi milioni 1,689,870, Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali shilingi milioni 907,370 na Utengenezaji wa Nguo shilingi milioni 323,108.



**Jedwali Na. 11: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2015**

Shughuli ya Kiwanda	(Shilingi Milioni)		
	Pato Ghafi	Gharama za Uzalishaji	Ongezeko la Thamani
Utengenezaji wa bidhaa za chakula	4,018,577	2,783,040	1,235,537
Utengenezaji wa vinywaji	1,943,061	853,724	1,089,337
Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku	649,878	195,188	454,690
Utengenezaji wa nguo	767,554	474,645	292,909
Utengenezaji wa mavazi	411,661	96,303	315,358
Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana	53,587	36,110	17,477
Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia	604,822	264,430	340,393
Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi	105,914	84,298	21,616
Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa	239,755	108,503	131,252
Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyo safishwa	56,863	49,599	7,264
Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali	635,446	373,463	261,982
Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea	74,633	40,109	34,525
Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki	538,599	299,471	239,128
Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali	1,130,866	608,484	522,382
Utengenezaji wa metali za msingi	251,930	164,183	87,748
Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa	296,279	112,986	183,293
Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni	12,541	6,636	5,905
Utengenezaji wa vifaa vya umeme	95,814	60,092	35,722
Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa	31,480	24,049	7,431
Utengenezaji wa magari na matela ya malori	36,281	11,416	24,866
Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri	70,560	51,845	18,715
Utengenezaji wa samani	424,211	217,409	206,802
Utengenezaji mwengine wa bidhaa vya viwandani	89,588	69,570	20,018
Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa	24,593	3,433	21,161
<b>Jumla</b>	<b>12,564,497</b>	<b>6,988,987</b>	<b>5,575,510</b>

**Jedwali Na. 12: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, ASIP 2016**


Shughuli ya Kiwanda	(Shilingi Milioni)		
	Pato Ghafi	Gharama za Uzalishaji	Ongezeko la Thamani
Utengenezaji wa bidhaa za chakula	6,552,690	3,956,411	2,596,278
Utengenezaji wa vinywaji	2,768,870	1,079,000	1,689,870
Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku	260,299	184,784	75,515
Utengenezaji wa nguo	353,711	193,757	159,954
Utengenezaji wa mavazi	433,259	110,151	323,108
Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana	62,317	41,943	20,374
Utengenezaji wa mbaao na bidhaa zitokanazo na mbaao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia	196,829	60,105	136,724
Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi	214,617	73,719	140,899
Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa	362,538	99,751	262,788
Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyo safishwa	49,287	43,710	5,578
Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali	618,251	315,118	303,133
Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea	139,110	89,130	49,979
Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki	462,321	235,428	226,893
Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali	1,532,643	625,273	907,370
Utengenezaji wa metali za msingi	261,959	193,283	68,675
Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa	498,378	254,333	244,045
Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni	29,619	14,558	15,061
Utengenezaji wa vifaa vya umeme	126,353	82,001	44,352
Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa	32,929	25,745	7,184
Utengenezaji wa magari na matela ya malori	64,315	48,129	16,187
Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri	98,044	11,660	86,384
Utengenezaji wa samani	314,808	157,682	157,126
Utengenezaji mwengine wa bidhaa vya viwandani	370,497	339,796	30,701
Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa	9,572	1,067	8,505
<b>Jumla</b>	<b>15,813,217</b>	<b>8,236,535</b>	<b>7,576,681</b>

### **5.3 Ongezeko la Thamani katika Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi.**

Kutokana na jumla la Ongezeko la Thamani la sekta ndogo ya Utengenezaji wa bidhaa Viwandani kwa mwaka 2015 ya shilingi million 5, 575,510, makundi yanayoongoza kwa kuwa na Ongezeko la Thamani kubwa ni, kundi la wafanyakazi mia moja hadi mia nne tisinin na tisa (100 – 499) lenye shilingi milioni 2,605,798 9asilimia 46.7) likifuatiwa na kundi lenye wafanyakazi mia tano au zaidi (500+) lenye shilingi milioni 1,201,128 (asilimia 21.5).

Mwaka 2016, kutokana na jumla la Ongezeko la Thamani la sekta ndogo ya Utengenezaji wa bidhaa Viwandani ya shilingi million 7,576,681, makundi yanayoongoza kwa kuwa na Ongezeko la Thamani kubwa ni, kundi la wafanyakazi mia moja hadi mia nne tisinin na tisa (100 – 499) lenye shilingi milioni 3,558,285 (asilimia 47.0 likifuatiwa na kundi lenye wafanyakazi mia tano au zaidi (500+) lenye shilingi milioni 2,035,054 (asilimia 26.9).

**Mchoro Na. 4: Mgawanyo wa Ongezeko la Thamani Katika Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara.**



#### **5.4 Ongezeko la Thamani katika Sekta ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa.**

Ongezeko la Thamani Ki-Mkoa linatofautiana kati ya mkoa na mkoa, matokeo yanaonyesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam ulichangia kiasi kikubwa zaidi ya mikoa mingine kwa kiasi cha shilingi milioni 3,081,893 (asilimia 55.3) ikifuatiwa na Arusha shilingi milioni 514,640 (asilimia 9.2); Mwanza shilingi milioni 327,683 (asilimia 5.9); Kilimanjaro shilingi milioni 325,516 (asilimia 5.8); na Pwani shilingi milioni 278,407 (asilimia 5.0). Mikoa hii mitano ilichangia jumla ya asilimia 81.2 ya ongezeko la thamani viwandani. Mikoa 20 ili yobaki ilichangia jumla ya asilimia 18.8 ya ongezeko la thamani yote viwandani.

Katika mwaka 2016, Ongezeko la Thamani Ki-Mkoa matokeo yanaonyesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam ulichangia kiasi kikubwa zaidi ya mikoa mingine kwa kiasi cha shilingi milioni 4,350,549 (asilimia 57.4) ikifuatiwa na Tanga shilingi milioni 508,109 (asilimia

6.7); Kilimanjaro shilingi milioni 407,748 (asilimia 5.4); Mwanza shilingi milioni 403,292 (asilimia 5.3); na Mbeya shilingi milioni 350,124 (asilimia 4.6). Mikoa hii mitano ilichangia jumla ya asilimia 79.4 ya ongezeko la thamani viwandani. Mikoa 20 iliyobaki ilichangia jumla ya asilimia 20.6 ya ongezeko la thamani yote viwandani.

**Jedwali Na. 13: Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani (MVA) Ki-Mkoa, Tanzania Bara, ASIP 2015 na 2016**

Mkao	2015		2016		(Million TZS)
	MVA	Asilimia	MVA	Asilimia	
Dodoma	48,232	0.9	94,812	1.3	
Arusha	514,640	9.2	321,913	4.2	
Kilimanjaro	325,516	5.8	407,748	5.4	
Tanga	180,405	3.2	508,109	6.7	
Morogoro	221,305	4.0	215,561	2.8	
Pwani	278,407	5.0	305,831	4.0	
Dar es Salaam	3,081,893	55.3	4,350,549	57.4	
Lindi	2,075	0.0	1,936	0.0	
Mtwara	27,132	0.5	72,143	1.0	
Ruvuma	25,213	0.5	14,550	0.2	
Iringa	88,798	1.6	172,095	2.3	
Mbeya	87,913	1.6	350,124	4.6	
Singida	10,193	0.2	12,590	0.2	
Tabora	71,301	1.3	69,445	0.9	
Rukwa	48,287	0.9	40,112	0.5	
Kigoma	6,697	0.1	6,761	0.1	
Shinyanga	118,171	2.1	68,977	0.9	
Kagera	29,153	0.5	32,117	0.4	
Mwanza	327,683	5.9	403,292	5.3	
Mara	22,033	0.4	35,236	0.5	
Manyara	20,570	0.4	16,779	0.2	
Njombe	16,136	0.3	32,023	0.4	
Katavi	2,095	0.0	6,888	0.1	
Simiyu	15,296	0.3	25,719	0.3	
Geita	1,835	0.0	1,266	0.0	
Songwe	4,528	0.1	10,103	0.1	
<b>Jumla</b>	<b>5,575,510</b>	<b>100</b>	<b>7,576,681</b>	<b>100.0</b>	